**Ni vipi teknolojia inakusaidia wewe, familia yako na jamii yako wakati huu wa janga la ugonjwa wa Korona?**
By Esther Kamau, Grade 5.

Shukrani kwa teknolojia, kwani imerahisisha maisha sana. Kama maisha yangekuwa hayana teknolojia yangekuwa magumu sana. Teknolojia ni matumizi ya sayansi na uhandisi ili kujenga mambo muhimu.

Teknolojia  hutumika kuunda na kushiriki tovuti, kwa ajili ya usafiri, kuona vipindi na mengi zaidi. Lakini ni jinsi gani inaweza kutusaidia katika janga hili la Korona?

Teknolojia inaweza kutusaidia katika njia mbalimbali. Njia moja ni kuwasiliana na marafiki. Wakati wa Korona,teknolojia inatusaidia kuwasiliana na marafiki bila kusafiri. Wakati kama huu ni jambo la muhimu sana kuwajulia hali wale unaowapenda, teknolojia inasaidia kuwasiliana nao bila kusafiri.

Teknolojia pia inatusaidia kuendelea kusoma kidijitali ili tusisahau kusoma na kutia bidii masomoni. Elimu ni muhimu sana kwa sababu itatusaidia ili tufanikiwe kimaisha. Pia teknolojia inasaidia walimu wetu kuweza kutufikia sisi kama wanafunzi bado tukiwa manyumbani nwetu.

Ukihitaji kununua vitu zakupika keki kama sukari, unga, mayai na poda ya kuoka lakini hautaki kwenda sokoni kwa sababu ya Korona, je, utafanya nini? Asante kwa teknolojia, unaweza kununuwa vitu mtandaoni ili usiende sokoni na kuvunja sheria umbali wa kijamii. Tuko na mitandao kadhaa ambao unaweza ukatumia kuagiza bidhaa zako bila kuondoka nyumbani, moja yao ni Jumia.

Teknolojia inatusaidia kujifunza jinsi ya kutumia tarakilishi na simu. Inatusaidia tusome ni vipi zina tengenezwa na ni vipi zina tumiwa. Ni muhimu kwa sababu wakati tunapokuwa tunatumia tarakilishi au simu, tutakuwa na ujuzi mwingi wa kutumia wakati wa kutumia tarakilishi na simu.

Jinsi nyingine ambayo teknolojia inatusaidia wakati huu wa janga la Korona ni kwa kupeperusha habari kupitia televisheni, redio au simu. Kwa mfano kama jamii tunapata kuelewe jinsi ya kujilinda kutoka kwa hili janga la korona kupitia hii mitandao. Serikali imeweza kuelimisha jamii kupitia kwa hii mitandao. Inatusaidia kujua kile ambacho serikali inatuambia tufanye ili kuepuka korona, kama kuvaa barakoa, kusafisha mikono, kuweka mita moja kutoka kwa mtu mwingine, kunawa mikono na kukohoa kwenye kiwiko chako.

Teknolojia inatusaidia kujifunza vitu ambavyo hatuvijuwi kama kupika au kuimba ama kutegeneza meza. Hii inaweza kuwa kwa ajili ya kujifurahisha au kujifunza kama ushindani huu wa “Digital essay competition”. Njia nyingine ambayo teknolojia imesaidia jamii ni kwamba, elimu ya Eneza imeshirikiana na Safaricom kutoa vifaa vya kujifunza bure kwa njia rahisi zaidi ya simu za mkononi, Ili watoto waendelee kusoma na kutia  bidii.

Njia ya saba ni, inasaidia wazazi wetu wafanye kazi nyumbani. Bila ya teknolojia, wazazi wetu hawangeweza kufanya kazi nyumbani. Matokeo yake, ni ya kwamba wazazi wetu hawangeweza kijikimu kimaisha wakati huu wa janga la Korona.

Shukrani kwa teknolojia, kuna tarakilishi na simu zinazosaidia wazazi kufanya kazi zao wakiwa nyumbani.

Teknolojia pia inatusaidia sisi kulipa pesa bila kushika pesa yenyewe na pia bila kusafiri sisi wenyewe. Siku hizi, watu hupenda kutumia "M-Pesa". M-pesa ni huduma ya simu kwa uhamisho wa fedha. Unaweza tumia  M-Pesa kutumia rafiki, wazazi au mtu yeyote pesa hata akiwa mbali na wewe. Teknolojia ilisaidia kutengeneza M-Pesa iliosaidia kufanya malipo bila kutumia noti na sarafu na inasaidia kupunguza maambukizi ya Korona. Kampuni kubwa ya mawasiliano ya nchi ya Kenya, Safaricom, imepunguza ada ya ubadilishanaji wa fedha na shughuli zote za mtu binafsi chini ya elfu moja shilingi ya Kenya ni bure kwa miezi mitatu.

Sasa kwa kuwa tumeona mambo ya manufaa kuhusu teknolojia, hebu tuzungumzie kuhusu hasara za teknolojia. Kuna hasara mbalimbali kama mashambulizi ya mtandao na utapeli.

Ni hatari kubwa sana kwa watu wote, watoto au watu wakubwa, watapeli wanaweza kusoma maelezo yako ya kibinafsi kama nenosiri la benki kisha kuiba pesa zako. Wanaweza hata kufuatilia ukitumia kompyuta au simu yako ili waweze kuiba au kufanya kitu kibaya kwako. Hiyo ndio sababu bado ni muhimu kuweka usalama mtandaoni wakati huu wa janga la Korona. Unaweza uliza mzazi wako au mtu ambaye unaamwamini akusaidie kuweka usalama ukiwa mtandaoni.

Tumeona ya kwamba teknolojia inaweza kutusaidia na njia nyingi sana wakati huu wa janga la ugonjwa wa Korona. Ni kwa jinsi gani unaweza kusaidia jamii yako kukomesha Korona?